**JUMUIYA YA UFUNDISHAJI WA MASOMO YA KIISLAMU TANZANIA (TISTA)**
**SAMPULI YA UPIMAJI WA KITAIFA WA DARASA LA NNE**

R**10** **ELIMU YA DINI YA KIISLAMU**

**Muda: Saa 1:30** **Mwaka: 2026**

***Majina matatu ya Mtahiniwa*** ____________________________________________
***Jina la Shule*** ______________________________________________________
***Mkoa*** __________________________________________________________
***Wilaya***__________________________________________________________

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenye jumla ya maswali **sita (6)**.
2. Jibu maswali **yote** katika nafasi ulizopewa.
3. Sehemu A ina alama **ishirini (20)** na sehemu B ina alama **thelathini (30)**.
4. Maandishi yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa **bluu** au **mweusi**.
5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** ndani ya chumba cha upimaji.
6. Andika **Majina yako matatu** na taarifa nyingine zote muhimu katika nafasi zilizowazi hapo juu.

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **SAHIHI YA MTAHINI** |
| 1 | | |
| 2 | | |
| 3 | | |
| 4 | | |
| 5 | | |
| 6 | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAHIHI YA MHAKIKI** | | |

## SEHEMU A (Alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Katika kipengele cha (i) – (x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi hiyo katika kisanduku ulichopewa.

(i) Mtume Muhammad (S.A.W) alipokuwa kijana mwenye tabia njema alimuoa Bi Khadija. Alikuwa na umri wa miaka mingapi?
A. 20  B. 25  C. 30  D. 35

(ii) Mwanafunzi mwenzako akikuuliza ni sehemu gani Mtume Muhammad (S.A.W) alipokea wahyi wa kwanza, utamtajia sehemu ipi?
A. Pango la Thawr  B. Msikiti wa Qubah
C. Pango la Hira  D. Mlima Uhud

(iii) Bilal (R.A) aliendelea kushikamana na Uislamu licha ya mateso makubwa aliyoyapata kutoka kwa wapinzani wa Uislamu. Hali hiyo inatufundisha nini?
A. Ujasiri katika dini
B. Kupenda mali
C. Kupenda ugomvi
D. Uvivu

(iv) Waislamu walipokabiliwa na mateso Makka walihamia Uhabeshi kutafuta amani. Nani alikuwa kiongozi wao?
A. Umar (R.A)
B. Abu Bakr (R.A)
C. Jaafar bin Abu Talib
D. Ali (R.A)

(v) Mtume Muhammad (S.A.W) alipelekwa Miiraj na akaoneshwa alama mbalimbali za Allah (S.W). Lengo kuu lilikuwa lipi?
A. Kupata mali  B. Kuimarisha imani yake
C. Kutembelea marafiki  D. Kufanya biashara

(vi) Israa ni safari aliyofanya Mtume Muhammad (S.A.W) kwa usiku mmoja, safari hiyo ilikuwa kutoka wapi hadi wapi?
A. Makka hadi Madina  B. Makka hadi Al-Aqswa
C. Madina hadi Makka  D. Makka hadi Uhud

(vii) Tukio la kuhama kutoka Makka kwenda Madina lilikuwa muhimu sana katika historia ya Uislamu. Tukio hilo linaitwaje?
A. Badri  B. Hijra  C. Hija  D. Fat-hu Makka

(viii) Vita vya Badri vinakumbukwa kwa funzo gani?
A. Ushindi unatoka kwa Allah (S.W)
B. Vilikuwa vita vya mwisho vya Waislamu
C. Vilifanyika Makka baada ya Hijra
D. Vilihusisha Warumi na Waajemi

(ix) Mtume (S.A.W) alifanya jambo gani muhimu katika kuanzisha Dola ya Kiislamu Madina?
A. Kujenga soko
B. Kuandika Katiba ya Madina
C. Kujenga nyumba yake
D. Kuanzisha biashara

(x) Mwenye kuwafundisha watu kumuabudu Allah (S.W), anafanya kazi inayofanana na kazi ipi ya Mitume?
A. Kufundisha Uislamu
B. Kulima mashamba
C. Kujenga nyumba
D. Kufanya biashara

2. Oanisha maelezo ya visomo vya Swala katika **Orodha A** na visomo husika katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi kwenye mabano.

| **Orodha A** | | **Majibu** | **Orodha B** |
|---|---|---|---|
| (i) | Kisomo kinachofungua Swala na kuashiria kuanza kwa ibada hiyo | (   ) | A. Kusoma Tahiyyatu<br>B. Kumswalia Mtume (S.A.W)<br>C. Takbira ya Kuhirimia<br>D. Kutoa Salamu<br>E. Kusoma Suratul-Faatiha<br>F. Kusoma Dua ya Qunut<br>G. Kusoma Sura baada ya Al-Faatiha |
| (ii) | Kisomo ambacho ni lazima kisomwe katika kila rakaa ya Swala | (   ) | |
| (iii) | Kuinama huku mikono ikiwa magotini na mgongo ukiwa sawa | (   ) | |
| (iv) | Kisomo kinachohusisha kumuombea rehema na amani Mtume Muhammad (S.A.W). | (   ) | |
| (v) | Kisomo kinachotamkwa mwishoni mwa Swala kuashiria kumalizika kwake | (   ) | |

3. Katika kipengele (i) – (v), chagua jibu sahihi kutoka katika mabano na kuliandika katika sehemu iliyoachwa wazi.

(i) Muislamu anashauriwa kuingia chooni kwa kutumia mguu upi?

_______________________________________________

(Mguu wa kulia, Mguu wa kushoto, Miguu yote miwili)

(ii) Muislamu anapovaa nguo safi anashauriwa kumshukuru Allah kwa kusema nini?

_______________________________________________

(Subhanallah, Allahu Akbar, Alhamdulillah)

(iii) Muislamu anapoingia msikitini anashauriwa kuanza kwa mguu upi?

_______________________________________________

(Mguu wa kushoto, Mguu wa kulia, Miguu yote miwili)

(iv) Salamu ya Kiislamu inayotumika kuwasalimia watu ni ipi?

_______________________________________________

(Marhaba, Assalamu alaykum, Tafadhali)

(v) Unapaswa kufanya nini unapomtembelea mgonjwa?

_______________________________________________

(Kumcheka, Kumsaidia na kumjulia hali, Kumwacha peke yake)

**SEHEMU B (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

4. Kwa kuzingatia Suratul Falaq, panga aya za sura hiyo katika mtiririko sahihi kwa kuandika herufi A-E chini ya namba za kirumi katika jedwali ulilopewa.

(i) Na shari ya mwenye husuda anapohusudu.
(ii) Kutokana na shari ya alivyoumba.
(iii) Sema: Ninajikinga kwa Mola wa mapambazuko.
(iv) Na shari ya wanaopulizia mafundo.
(v) Na shari ya giza linapoingia.

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |

5. Andika majibu kwa ufupi katika sehemu iliyoachwa wazi.

(a) Katika umbile la mbingu na ardhi kuna dalili zinazothobitisha kuwepo kwa Allah (S.W). Taja dalili mbili.

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

(b) Orodhesha dalili mbili zinazopatikana katika umbile la ardhi zinazothibitisha kuwepo kwa Allah (S.W)

(i) ______________________________

(ii) ______________________________

(c) Eleza dalili moja inayothibitisha kuwepo kwa Allah (S.W) kutokana na nafsi ya mwanadamu

______________________________

______________________________

______________________________

(d) Eleza maana ya jina la Allah (S.W) la *As-Salaam*

______________________________

______________________________

______________________________

(e) Allah (S.W) ana majina mazuri yanayopaswa kutumiwa na mwanadamu. Bainisha matumizi ya majina hayo ya Allah (S.W)

______________________________

______________________________

______________________________

6. Kamilisha aya ifuatayo kwa kuandika maneno yanayokosekana katika nafasi zilizotolewa katika vipengele (i)–(v).
Kutawadha ni mojawapo ya masharti muhimu ya Swala. Miongoni mwa nguzo za kutawadha ni kuwa na (i) ____________________, kuosha (ii) ____________________, kuosha (iii) ____________________, kupaka maji (iv) ____________________, na kuosha (v) ____________________.